**OFISI YA RAISI**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**SHULE YA SEKONDARI DUMILA**


KUMB.NA.DSS/ADM/VOL.1/20/..............
SIMU: Mkuu wa shule 0717728984
Makamu wa shule 0784557345
Mtaaluma 0763834870/0755386135

Shule ya Sekondari Dumila,
S. L. P 120,
Morogoro.


15/12/2020

MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI..........................................................................
NAMBA YA SIMU...................................................................

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI DUMILA MWAKA 2021**

## 1.0 UTANGULIZI

- Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021
- Shule ya Sekondari Dumila ipo umbali wa kilometa tano kutoka njia panda ya kwenda Kilosa. Usafiri wa kutoka Dumila kuja shuleni unapatikana katika kituo kidogo cha mabasi cha Dumila. Nauli kwa pikipiki ni Tsh 1500/= na bajaji ni Bajaji ni Tsh. 500/=.
- Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe 11/01/2021 SIKU YA JUMATATU. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 11/01/2021. Mwisho wa kuripoti ni tarehe 25/01/2021.
- NI MARUFUKU KWA MWANAFUNZI YEYOTE KUMILIKI SIMU YA MKONONI SHULENI

## 2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### A. SARE ZA SHULE KWA WAVULANA

- Suruali mbili (02) za kitambaa rangi ya maruni na shati (02) za rangi nyeupe aina ya tomato zilizoshonwa kwa heshima. Marufuku mshono wa JEANS AU MLEGEZO , AU suruali inayobana (**MODO**). (KITAMBAA KIMEAMBATISHWA).
    - Mashati mawili meupe ya mikono mifupi yasiyoangaza.
    - Suruali

Scanned with CamScanner

        - iwe na marinda mawili kulia na mawili kushoto,
        - isiwe ya kubana yaani "Model" upana chini usipungue wala kuzidi sentimeta 16.
- Viatu vya ngozi jozi mbili (02), rangi nyeusi vya kamba na vyenye kisigino kifupi.
    - Buti, raba na viatu vya kuchomeka haviruhusiwi kabisa.
- Soksi jozi mbili rangi nyeusi
- Mkanda wa suruali – rangi nyeusi (usio na urembo)
    - Usiwe mkanda wa utambi
- Fulana moja (01) rangi ya njano lisilo na kola lenye nembo ya shule atakalovaa mwanafunzi siku ya jumatano (LINAPATIKANA SHULENI).
- Sweta moja (01) rangi ya maruni (reddish brown) lenye shingo ya V.

## B. SARE ZA SHULE KWA WASICHANA

- Sketi mbili (02) za kitambaa rangi ya maruni na shati (02) za rangi nyeupe aina ya tomato zilizoshonwa kwa heshima. Marufuku mshono wa JEANS AU MLEGEZO , AU SKETI FUPI (**KIMINI**). (KITAMBAA KIMEAMBATISHWA).
    - Mashati mawili meupe ya mikono mifupi yasiyoangaza.
    - Sketi
        - ziwe za rinda box matatu kulia na matatu kushoto,
        - ziwe za urefu wa inchi kumi (10") toka miguuni kuelekea kwenye goti.
- Viatu vya ngozi jozi mbili (02), vyenye rangi nyeusi, vya kufunga kamba, vyenye kisigino kifupi na visiwe na urembo wowote.
    - Buti, raba na viatu vya kuchomeka na visivyo na kamba haviruhusiwi kabisa.
- Soksi jozi mbili rangi nyeupe na zisiwe na urembo au alama yoyote ya rangi.
- Fulana moja (01) rangi ya njano lisilo na kola lenye nembo ya shule atakalovaa mwanafunzi siku ya jumatano (UTAELEKEZWA LINAPOPATIKANA).
- Sweta moja (01) rangi ya maruni (reddish brown) lenye shingo ya V (UTAELEKEZWA LINAPOPATIKANA).

NB: Wasichana wa kiislamu wanaruhusiwa kuvaa hijabu kama ifuatavyo:-
    - Sketi ndefu inchi sita (6") kutoka miguuni, rangi ya maruni
    - Nusu kanzu nyeupe mikono mirefu
    - Kijuba/mtandio mweupe usio na urembo au alama yoyote.
    - Fulana moja (01) rangi ya njano lisilo na kola lenye nembo ya shule atakalovaa mwanafunzi siku ya jumatano pamoja na Kijuba/mtandio wa njano usio na urembo au alama yoyote.

## C. SARE ZA MICHEZO

- Jezi moja (01); bukta moja (01) na fulana moja (01) rangi nyekundu au bluu
- Traki suti moja (01) rangi ya nyekundu au bluu

Scanned with CamScanner

- Raba ya michezo jozi moja (01) na viatu vya kuchezea mpira wa miguu
- Soksi za michezo rangi nyekundu au bluu

o

**2.1 VIFAA VYA MASOMO**

- Madaftari 12 aina ya Counterbook Q3/Q4
- Kalamu na mkebe kwa masomo ya sayansi na hesabu
- Daftari kwa ajili ya mazoezi(Test) kila somo lako

**2.2 MAHITAJI MENGINE**

- Cheti cha kuzaliwa (birth certificate) ni muhimu aje nacho
- Picha za passport size za wazazi/walezi zitawekwa kwenye file la mwanafunzi.

**3.0 SHERIA ZA SHULE**

- Shule hii inaendeshwa kwa mujibu na kanuni, za Elimu ya 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara zenye dhamana ya Elimu nchini.
- Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:-
  - ✓ Mwanafunzi anapaswa kuwa na Heshima, mtiifu, na mwenye adabu wakati wote kwa walimu na wafanyakazi wasio walimu, wazazi, viongozi mbalimbali. Ukaidi na dharau kwa viongozi ni marufuku.
  - ✓ Mwanafunzi unatakiwa kuvaa sare rasmi ya shule muda wote wa shule (Darasani) isipokuwa muda wa kazi za nje na michezo (utavaa nguo za michezo)
  - ✓ Mwanafunzi ni lazima uwahi popote unapotakiwa na kwa wakati uliowekwa
  - ✓ Mwanafunzi ni lazima aheshimu kazi za darasani na nje na kuzifanya vizuri. Ni lazima kufanya mazoezi/ mitihani yote inayotolewa darasani.
  - ✓ Lugha chafu , matusi, ugomvi, fitina na kupigana kwa mwanafunzi ni mwiko kabisa.
  - ✓ Unywaji wa pombe , uvutaji wa aina yeyote ya sigara au madawa ya kulevya ni mwiko kwa mwanafunzi. Hairuhusiwi kufanya yoyote shuleni.
  - ✓ Wizi wa aina yoyote ni marufuku nani kosa kubwa kwa mwanafunzi.
  - ✓ Uharibifu na upotevu mali ya binafsi na umma pia ni kosa kubwa.
  - ✓ Mwanafunzi haruhusiwi kuoa wakati akiwa bado shule; Akibainika atafukuzwa shule mara moja. Aidha ni marufuku kuwa na mahusiano ya mapenzi awapo shuleni. Akibainika atafukuzwa shule.

**4.0 MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

- ✓ Wizi wa aina yoyote ile,
- ✓ Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa /utoro
- ✓ Kugoma kuhamasisha mgomo

Scanned with CamScanner

- ✓ Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla
- ✓ Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote
- ✓ Kufuga ndevu
- ✓ Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
- ✓ Uvutaji wa sigara
- ✓ Uasherati, uhusiano wa jinsi moja , kuoa au kuolewa
- ✓ Kushiriki matendo ya uhalifu , siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
- ✓ Kusababisha mimba, kupata mimba, kutoa au kushiriki kutoa mimba
- ✓ Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
- ✓ Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule
- ✓ Kudharau Bendera ya taifa
- ✓ Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
- ✓ Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

...........................................

**ODILO R. MWOMBEKI**

**MKUU WA SHULE**

HEADMASTER
DUMILA SECONDARY SCHOOL
P.O. Box 120, MOROGORO

Scanned with CamScanner

FOMU C.1

# SHULE YA SEKONDARI YA DUMILA

## FOMU YA TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI NA KUKUBALI SHERIA NA NAFASI YA SHULE ALIYOPEWA

picha

### 1. TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI

- Jina kamili la mwanafunzi.........................................................................
- Tarehe ya kuzaliwa...............(ambatanisha nakala ya cheti cha kuzaliwa)
- Mahali alipozaliwa (Mkoa na Wilaya)
- Uraia: MTANZANIA/SIYO MTANZANIA
- Shule uliyotoka.......................................................................................
- Namba ya mtihani **(S..**..................................)

### 2. TAARIFA YA MZAZI/MLEZI

- Jina la mzazi/mlezi...................................................................................
- Kazi ya mzazi/mlezi..................................................................................
- Anuani ya mzazi/mlezi...............................................................................
- Simu ya mzazi/mlezi – kazini......................... nyumbani.........................

  Mkononi.........................................................

  (kama huna nambari ya simu, ya jirani yako

  ..............................................................................

### 3. MWANAFUNZI

Mimi ...................................... nimesoma na kuyaelewa maelekezo yote kwa hiyo nakubali kuipokea/sikubali kuipokea nafasi niliyopewa. Ninaahidi kufuata sheria na taratibu zote za shule na kujifunza kwa bidii.

Tarehe..................................... Sahihi.....................................................

### 4. MZAZI/MLEZI:

Nimehakikisha mwanangu amezisoma na kuzielewa sheria za shule name nimemsisitiza katika hilo.

Tarehe..................................... Jina ....................................................

Saini......................................

Scanned with CamScanner

**FORM B**

**DUMILA SECONDARY SCHOOL**

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

***FORM:*** The Medical Officer,
Government Hospital……………..
………………………
………………………
………………………

***TO:*** The Headmaster,
Dumila Secondary School,
P. O. Box 120,
**Morogoro.**

**RE: MEDICAL CERTIFICATE**
**(TO BE COMPLETED BY A GOVERNMENT MEDICAL OFFICER)**

I have examined……………………………………. who aspires to join Form I in your school as follows:-

| **AREA** | **REMARKS** |
|---|---|
| 1. Skin | ………………………………………………………… |
| 2. Eyes | ………………………………………………………… |
| 3. Ears | ………………………………………………………… |
| 4. Teeth | ………………………………………………………… |
| 5. Chest | ………………………………………………………… |
| 6. Spleen | ………………………………………………………… |
| 7. Abdomen | ………………………………………………………… |
| 8. Urine | ………………………………………………………… |
| 9. Stool | ………………………………………………………… |
| 10. HB Haemoglobin | ………………………………………………………… |
| 11. Innoculation againt meningitis | ………………………………………………………… |
| 12. Sickle cell | ………………………………………………………… |
| 13. Asthma | ………………………………………………………… |
| 14. Any other comments | ………………………………………………………… |

I consider that he/she* is physically/not physically fit to join your school.
Signature……………………………………….
Date…………………………………………….
Official stamp………………………………….

**Delete as necessary*

Scanned with CamScanner